

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

BUNGE LA TANZANIA



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA NANE

06 JUNI, 2022



ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

MKUTANO WA SABA

KIKAO CHA THELATHINI NA NANE – TAREHE 06 JUNI, 2022

I. DUA:

II. HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:

WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:

Randama za Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Fedha na Mipango kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Hotuba ya Bajeti ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HUDUMA NA MAENDELEO YA JAMII:

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Huduma na Maendeleo ya Jamii kuhusu utekelezaji wa majukumu ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2021/2022 pamoja

na Maoni ya Kamati kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara hiyo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

III. MASWALI:

OFISI YA RAIS (TAMISEMI):

335. MHESHIMIWA HASSAN ZIDADU KUNGU (TUNDURU KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

- Je, ni lini Serikali itapeleka shilingi milioni 500 ya ujenzi wa Kituo cha Afya Namiungo na milioni 200 ya Kituo cha Afya Nakayaya.

336. MHESHIMIWA ENG. EZRA JOHN CHIWELESA (BIHARAMULO MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais (TAMISEMI):-

Je, ni lini Serikali itajenga Jengo jipya la Halmashauri ya Wilaya ya Biharamulo.

WIZARA YA KATIBA NA SHERIA:

337. MHESHIMIWA ELIBARIKI IMMANUEL KINGU (SINGIDA MAGHARIBI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, ni lini Serikali itawasilisha Muswada wa Sheria unaozuia kukamata na kuwashikilia Watuhumiwa kabla ya kukamilisha upelelezi.

338. MHESHIMIWA NEEMA KICHIKI LUGANGIRA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Katiba na Sheria:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kupitia Sheria zinazokinzana na Sheria Namba 4 na 5 juu ya umiliki wa ardhi kwa Wanawake.

WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:

339. MHESHIMIWA MAIMUNA SALUM MTANDA (NEWALA VIJINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni lini Serikali itajenga mabweni pamoja na miundombinu mingine katika Chuo cha VETA Kitangari.

340. MHESHIMIWA FAKHARIA SHOMAR KHAMIS (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia:-

Je, ni Vijana wangapi wamepata nafasi za masomo nje ya nchi kwa Mwaka 2015 – 2020 na kati yao ni wangapi wanatoka Zanzibar.

WIZARA YA UWEKEZAJI, VIWANDA NA BIASHARA:

341. MHESHIMIWA ATHUMAN ALMAS MAIGE (TABORA KASKAZINI):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kujenga Viwanda vya Mbolea nchini ili Wakulima waongeze tija.

WIZARA YA NISHATI:

**342. MHESHIMIWA ANTON ALBERT
MWANTONA (RUNGWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nishati:-

Je, ni lini Mradi wa REA II wenye Vijiji 25 na REA III wenye Vijiji 33 utakamilika katika Jimbo la Rungwe.

IV. HOJA ZA SERIKALI:

WAZIRI WA UTAMADUNI, SANAA NA MICHEZO:

Kwamba, Bunge sasa likubali kupokea na kupitisha Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Utamaduni, Sanaa na Michezo kwa Mwaka wa Fedha 2022/2023.

**DODOMA
06 JUNI, 2022**

**N.J. MWIHAMBI, *ndc*
KATIBU WA BUNGE**